

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TANO

KIKAO CHA SABA

08 NOVEMBA, 2016



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TANO

KIKAO CHA SABA – TAREHE 08 NOVEMBA, 2016

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

**69. MHESHIMIWA NEEMA WILLIAM MGAYA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Vijana wengi Nchini wanakabiliwa na tatizo kubwa sana la ukosefu wa ajira:-

Je, Serikali imejipanga vipi kutatua tatizo hilo.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**70. MHESHIMIWA HUSSEIN MOHAMMED BASHE
(NZEKA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali inakusudia kuanza utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya Kilomita 10 ndani ya Mji wa

Nzega kama ambavyo Mheshimiwa Rais aliahidi wakati wa Kampeni.

71. MHESHIMIWA IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI (KIEMBE SAMAKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Serikali imeanzisha mabasi yaendayo kwa kasi katika Jiji la Dar es Salaam lakini Madereva wengi wamekuwa wakiendesha magari hayo kwa kasi kubwa kiasi cha kuhatarisha maisha ya watu waendao kwa miguu:-

- (a) Je, ni lini Serikali itawachukulia hatua Madereva ambao hawafuati Sheria za barabarani;
- (b) Je, ni muda gani magari hayo ya DART yamepangiwa kuanza kazi na muda wa kumaliza kazi.

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

72. MHESHIMIWA DKT. PUDENCIANA WILFRED KIKWEMBE (KAVUU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, kwa nini Serikali ya Watu wa Jamhuri ya China wasichangie huduma za afya kwa Wananchi wanaopata ajali zinazotokana na waendesha bodaboda.

73. MHESHIMIWA FATMA HASSAN TOUFIQ:

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Tatizo la ukeketaji katika Jamii nyingi nchini bado ni kubwa na sasa ukeketaji huo unafanywa kwa usiri mkubwa hasa baada ya Jamii hizo kugundua kuwa ipo sheria dhidi ya ukeketaji:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kufuatilia ukatili huu wanaofanyiwa Watoto Wachanga na kuhatarisha maisha yao;
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwanusuru Watoto Wachanga dhidi ya ukatili huu wa ukeketaji unaofanywa na baadhi ya Jamii nchini.

WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

74. MHESHIMIWA AUGUSTINO MANYANDA MASELE (MBOGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Kwa kuwa Jimbo la Mbogwe limejaaliwa kuwa na madini ya dhahabu na utafiti umekuwa

ukiendelea bila uchimbaji kufanyika katika maeneo ya Nyakafuru, Kenegere n.k.:-

Je, ni lini Wizara ya Nishati na Madini itayaachia maeneo haya na kuyagawa kwa wachimbaji wadogo.

75. MHESHIMIWA MARTIN ALEXANDER MTONDA MSUHA (MBINGA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Wananchi wa Mbinga wanaishukuru Serikali kwa mradi wa kusambaza umeme Vijijini kwani wanaimani mradi huo utasaidia kuinua hali za maisha. Hata hivyo ni Vijiji 34 tu ndio vimepatiwa umeme kupitia mpango wa usambazaji umeme unaotekelezwa na REA awamu ya pili:-

Je, lini Serikali itapeleka umeme katika Vijiji 118 vilivyosalia.

WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

76. MHESHIMIWA GIBSON OLE - MEISEYEKI (ARUMERU MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Wakulima na Wafugaji wa Tanzania hawajawahi kuwa na uhakika wa bei

ya mazao yao hasa katika msimu wa mavuno ya kutosha badala yake wanageuka watumwa wa mazao yao wenyewe kwa kukosa masoko, maghala na bei nzuri ya mazao yao:-

Je, ni lini tatizo hili litaisha ili kuwezesha Watanzania wengi kujiingiza kwenye Kilimo na Ufugaji.

77. MHESHIMIWA GIMBI DOTTO MASABA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Kutokana na mpango wa Serikali kuhakikisha ifikapo mwaka 2025 Tanzania inafikia uchumi wa kati:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha na kuhalalisha viwanda vya kutengeneza pombe aina ya gongo ili kuchochea uchumi wa nchi;
- (b) Pombe hii aina ya gongo inapendwa kunywewa zaidi na watu wa vijijini, Je, Serikali haioni kwamba umefika wakati wa kuwaendeleza kielimu zaidi ili wataalam hao wanaotengeneza pombe hiyo ili wapate ujuzi kwa maslahi ya Taifa.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

78. MHESHIMIWA SALMA MOHAMMED MWASSA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, ni nini umuhimu wa kuwa na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya katika Nchi hii.

III. MKATABA WA UBIGIA WA UCHUMI BAINA YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI NA UMOJA WA ULAYA (EAC – EU EPA):

IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2016 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2016).*

**DODOMA
08 NOVEMBA, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**